



KATC Taarifa

Umwagiliaji Maji Mashambani Kwa Maendeleo ya Kilimo

Toleo na. 2

Aprili-Juni 2004



WIZARA YA KILIMO NA CHAKULA
KILIMANJARO AGRICULTURAL TRAINING CENTRE (KATC)-MOSHI
S.L.P 1241 MOSHI- Simu 255-27-2752293

Mradi wa KATC Awamu ya Pili wafanyiwa tathimini ya awali

*R. G. Shayo

Mradi wa KATC Awamu ya Pili umefanyiwa tathimini ya awali (ambayo hufanyika katikati ya kipindi cha muda wa utekelezaji) tarehe 20/5/2004 hadi 24/5/2004.

Tathimini hiyo ambayo ilifanywa na wataalam kutoka JICA wakiongozwa na Bwana Ryuzo KAWAKAMI, na kutoka Wizara ya Kilimo na Chakula wakiongozwa na Eng. Gabriel M. Kalinga, ilichukua siku tano za mahojiano na wakufunzi wa KATC, kutembelea skimu ya mfano ya Mombo, na kufanya mahojiano na viongozi wa Wizara ya Kilimo na Chakula.

Taarifa ya kazi hiyo iliwasilishwa katika kikao cha nne cha Kamati ya Kuratibu shughuli za Mradi cha tarehe 25/5/2004. Baada ya maswali na majibu, Mwenyekiti wa Kamati, Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo na Chakula, Bw. Wilfred Ngirwa pamoja na kiongozi wa timu iliyofanya tathimini, Bw. Ryuzo KAWAKAMI waliweka sainsi zao kuthibitisha kwamba wameridhia matokeo ya tathimini hiyo. Ufuatao ni muhtasari wa yale yaliyopendekezwa ndani ya taarifa hiyo.

1. Kuwepo kwa mradi huu bado ni muhimu ili kuwaongezea wakulima elimu ya kilimo cha umwagiliaji kwa ufanisi katika skimu zao.

2. Timu ya kufanya tathimini imeridhika kwamba mradi umeendelea kutekelezwa kama ilivyokusudiwa. Ingawa kuna skimu chache za mfano ambazo shughuli za Mradi zimekwamishwa na hali ya hewa isiyoridhisha hususani ukame katika baadhi ya sehemu.

3. Ingawa mradi umeanza kuonyesha mafanikio, bado KATC hajawezeshwa vya kutosha na Serikali ili iweze kufanya kazi kubwa kama hii bila kutegemea msaada kutoka nje. Timu imeshauri kwamba Serikali ya Tanzania itumie kikamilifu rasilimali ya wataalam na vifaa vilivyowekezwa KATC kwa kukipa Chuo fedha za kutosha.

4. Timu ya kufanya tathimini ilipendekeza vile-vile mambo kadhaa yazingatiwe ili mradi uweze kufikia malengo ifikapo Septemba 2006. Baadhi ya hayo mambo ni kama vile:

• Sehemu za mkakati wa utekelezaji zirekebishwe kwa kutumia takwimu halisi badala ya zile zilizopo ambazo ni makadirio.



Katibu mkuu wa Wizara ya Kilimo na Chakula Mhe. Wilfred Ngirwa na kiongozi wa timu ya tathimini Bw. Ryuzo KAWAKAMI wakiweka sainsi taarifa ya tathimini ya mradi wa KATC awamu ya pili

- Wakulima wa Skimu ya Nduguti ambayo imeathiriwa sana na ukame wasaidiwe kuendelea kupata mafunzo katika skimu ya mfano ya Mwa-mapuli ambayo iko wilaya jirani.
- Chuo kiwe na mawasiliano ya karibu na Halmashauri za Wilaya ili wilaya zivutiwe kukitumia kuendesha mafunzo kwa wakulima.

Chuo kinawashukuru wadau wote wa Mradi wa KATC Awamu ya Pili hususan wakulima na viongozi wote wa Skimu za mfano pamoja na Halmashauri za wilaya husika, kwa ushirikiano mzuri uliowezesha mradi kufanikiwa. Tunatoa wito wa kuendelea na kazi hiyohiyo kwani kazi iliyoko mbele yetu bado ni kubwa.

Yaliyomo katika toleo hili:

- | | |
|--|-------|
| • Migogoro katika skimu za umwagiliaji | Uk. 2 |
| • Wakulima wa Nduguti wafanya ziara ya mafunzo | Uk. 3 |
| • Lishe bora | Uk. 3 |
| • Utayarishaji wa mbegu za mpunga | Uk. 4 |

Kwa wasomaji wetu:

Kuanzia toleo hili la pili katika ukurasa wa nne tutakuwa tunawaletea makala maalum ya mbinu za msingi za kilimo bora cha mpunga kwa njia ya umwagiliaji.

Mhariri

*Mkuu wa chuo

MIGOGORO KWENYE SKIMU ZA UMWAGILIAJI MAJI MASHAMBANI

Petet Mawete

Migogoro mingi iliyopo ndani ya skimu za umwagiliaji hutokana na kutoelewana kati ya mtu na mtu, mtu na kikundi au jumua, kikundi na kikundi kingine kutokana na kutofautiana katika msimamo wa kisiasa, itikadi, au kushindania matumizi ya rasilimali muhimu zilizopo kwa mfano maji, ardhi, n.k.

Aidha baadhi ya sababu zisababishazo migogoro ndani ya skimu za umwagiliaji ni pamoja na wakulima kupenda kukidhi mahitaji yao binafsi bila kujali mahitaji ya watu wengine (upendeleo katika ugawaji wa maji), Upungufu wa rasilimali muhimu kama maji na ardhi, pamoja na kukosekana au kutofuatwa kwa sheria ndogo ndogo zinazotawala ugawaji wa maji na mawasiliano duni.



Mifugo (Ng'ombe) wakichunga karibu na miundo mbinu ya umwagiliaji

Mara nyingi inakuwa vigumu kumaliza migogoro mara moja, hata hivyo ni vyema wahusika wakajaribu kumaliza migogoro hatua kwa hatua. Msaada kutoka kwenye utawala au vyombo vya sheria ni muhimu katika kushughulikia migogoro.

Zipo hatua ambazo kama zitawekewa mikakati maalumu ya utekelezaji husaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza kama sio kumaliza migogoro hiyo. Hatua hizo ni:

- Kufanya mikutano inayohusisha wadau wote ili kubaini chanzo cha tatizo.
- Watu wote kushirikiana katika kutoa ufumbuzi na maamuzi.
- Kufuata maamuzi yaliyotolewa na kikao.
- Kufanya ufuatiliaji kwa vikundi na wadau



Bwawa la maji linalotumiwa na skimu ya Mwamapuli. Rasilimali hii hutumiwa pia kwa matumizi ya nyumbani na mifugo.

wote wanaohusika pamoja na

- Kuwepo kwa sheria ndogo ndogo na ziwe zinafuatiliwa

Katika kufanikisha hatua hizo mambo yafuatayo hayana budi yazingatwe; Wakulima wanatakiwa kujadili jinsi ya kumwagilia kwa usawa na kufanya marekebisho au kutengeneza ratiba za umwagiliaji. Mgawanyo wa maji uzingatie eneo linaloweza kumwagiliwa kulingana na maji yaliyopo. Wakulima wajulishwe ratiba ya umwagiliaji kwa njia ya mbao za matanzgazo, mikutano ya vikundi vya umwagiliaji au mkutano mkuu n.k. Eneo linalomwagiliwa liongezwe tu baada ya kufanyika uchunguzi na makubaliano kati ya wahusika wote. Kama ni muhimu kuongeza kijengo kama vile mi-



Ng'ombe wakichunga ndani ya mashamba ya umwagiliaji

lango ya maji ili kuboresha udhibiti ni muhimu ukafanyika kwa haraka kabla ya msimu kuanza. Kwa migogoro

ihusuyo wakulima na wafugaji, wafugaji waelimishwe juu ya madhara yanayosababishwa na mifugo (Mifugo inapoingia kunywa maji au kukatisha kwenye mifereji husababisha uharibifu wa miundo mbinu na mazao). Ni muhimu pia kuwepo na sheria ya kudhibiti mwenendo wa mifugo pamoja na kujenga miundo mbinu kwa ajili ya huduma za mifugo - mfano, mabirika ya kunywesha mifugo, vuvuko na njia za mifugo.

Kwa kuzingatia mambo yote yaliyoelezwa hapo juu upo uwezekano mkubwa wa kupunguza migogoro inayoweza kutokea mara kwa mara katika skimu zetu za umwagiliaji. Migogoro hiyo kama haitatatuliwa haraka iwezekanavyo inaweza kusababisha skimu za umwagiliaji kudorora na hivyo kutoweza kufikia malengo ya uzalishaji yaliyokusudiwa.



Sehemu ya miundo mbinu ya umwagiliaji iliyo-haribiwa kutokana na upitishwaji wa mifugo

WAKULIMA WA NDUGUTI WAPATIWA MAFUNZO YA KILIMO BORA CHA MPUNGA KWA NJIA YA UMWAGILIAJI LICHA YA UKAME ULIWAKUMBA

Hanif Nzully

Katika msimu wa kilimo wa mwaka 2003/2004, Mradi wa KATC Awamu ya Pili ume-fanikiwa kuendesha mafunzo ndani ya skimu zote za mfano isipokuwa skimu ya Nduguti, ambayo ime-kumbwa na ukame. Hatua zote nne za mafunzo zilitekelezwa katika skimu tano za mfano (Mombo, Mwega, Mbuyuni, Nakahuga na Mwamapuli). Ukame huo ulisababisha skimu ya Nduguti ipate mafunzo mara moja tu.

Hata hivyo huzuni ya wakulima wa Nduguti iligeuzwa kuwa furaha wakati Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini ilipoamua kuwasafirisha wakulima viongozi 20 na wakulima wa kati 40 hadi skimu ya Mwamapuli, wilaya ya Igunga kuungana na wakulima wenzao ambao walikuwa wakiendelea na mafunzo ya hatua ya tatu na ya nne kama iliyopangwa, kwa vile skimu hiyo inalo bwawa la kuhifadhi maji ya kuwagilia.

Hakika hii ilikuwa ni fursa ya pekee kwa wakulima wa skimu ya Mwamapuli kuanza kazi ya kusambaza teknolojia ya kilimo bora cha mpunga

kwa njia ya umwagiliaji kwa wakulima kutoka skimu nyingine. Kazi hii waliifanya kwa furaha, wakiishi na wakulima wenzao majumbani mwao na kubadilishana mawazo na uzoefu katika kipindi chote cha mafunzo.

Kwa upande mwingine, ziara hiyo ya mafunzo ilikuwa ni changamoto kubwa kwa wakulima wa Nduguti ambao wamenuia kuitumia elimu waliyopata kikamilifu mara tu watakapoanza tena kupata mvua msimu ujao na kuthibitisha kauli mbiu yao inayosema **“Nduguti ni maendeleo na maendeleo ni Nduguti....hakuna kulala!!!!”** Mambo hayo.

Nasi KATC tunawasubiri kwa hamu ili tuthibitishwe kwa mara nyingine kwamba **“elimu kwa wakulima kupitia wakulima”** ni mbinu ya uhakika ya kuleta mabadiliko vijijini.



Wakulima wa Nduguti wakiwa na wenzao wa Mwamapuli wakati wa siku ya Wakulima iliyofanyika katika skimu ya Mwamapuli



Wakulima wa Nduguti wakiwasilisha waliyojifunza kwa wenzao baada ya kurudi toka ziarani Mwamapuli



LISHE BORA

Albertina Mushumba



Pamoja na KATC awamu ya pili kutilia mkazo kilimo bora cha mpunga na mazao mengine kwa njia ya umwagiliaji pia haijaaacha kutilia mkazo masuala ya lishe bora kwa wakulima.

Lishe bora ni chakula ambacho kina viini lishe vyote ambawo vinahitajika mwilini mwa bi-nadamu katika kiwango cha kutosheleza mahitaji ya mwili. Lishe bora huchangia kwa kiasi kikubwa kujenga kinga ya mwili ya kupambana na maradhi

mbalimbali.

Kutokula chakula bora kwa watoto na watu wazima huchangia kudhoofika kwa mwili hivyo kuathiri utendaji wa kazi za uzalishaji katika mashamba.

Idadi ya milo kwa siku kwa mtu ni kitu cha muhimu katika kuhakikisha kuwa mwili unapata kiwango sahihi cha lishe. Milo mitano 5 ndiyo inayotakiwa kwa mtu mzima kwa siku na isipungue milo mitatu (3) kwa siku yaani asubuhi, mchana na jioni.

Ili kuhakikisha kuwa lishe bora inapatikana ni muhimu kuzingatia mambo yafuatayo:

- Maandalizi yote ya chakula yafanyike katika hali ya usafi
- Kuwa na ratiba maalum ya muda wa kula na kuifuata
- Chakula au milo ibadilishwe mara kwa mara kama hali ya kiuchumi inaridhisha



Wakulima wa skimu ya Mbuyuni wakijifunza jinsi ya kuandaa na kupika mboga za majani

-Mboga za majani zisipikwe muda mrefu na wala zisiungwe na nyanya ili kuepuka upotevu wa vitamini c.

-Maji ya kunywa ni muhimu katika mwili. Lita moja ya maji kwa siku ndio kiwango kinachoshauriwa.

Hivyo basi ni muhimu kuzingatia lishe bora ili kuboresha afya zetu na hatimaye kuboresha ufanisi wa kazi.



Wakulima wa skimu ya Mwamapuli wakijifunza jinsi ya kuandaa na kupika mboga za majani



JINSI YA KUANDAA MBEGU ZA MPUNGA

Kitengo cha Kilimo bora cha mpunga-KAFC



Wakulima wengi wa mpunga wamekuwa wakitumia mbegu nyingi za mpunga ambazo huoteshwa na kupandwa bila kufahamu mahitaji halisi na kusababisha uharibifu wa mbegu usio wa lazima. Aidha miche ambayo hutokana na mbegu hizo huwa midhaifu na hivyo huchangia kuathiri uzalishaji. Hayo yote husababishwa na wakulima kutokujua mbinu bora za kitaalamu za utayarishaji wa mbegu za mpunga.

Ili kupata mbegu nzito na zilizojaa vizuri, hatua zifuatazo zinashauriwa zifuatwe: Kabla ya kusia mbegu kwenye kitalu, pembua na loweka mbegu ili kuondoa mapepe na kupata mbegu zilizojaa vizuri. Kuna njia mbili za kupembua mbegu nazo ni : kupembua kwa kutumia maji safi na kupembua kwa kutumia maji safi na chumvi. Katika njia hizo mbili; njia ya kupembua kwa maji yenye chumvi, ndiyo inayopendekezwa na wataalamu. Njia hii husababisha kiasi kikubwa cha mapepe kutoka ambayo yasingeweza kuondolewa kwa kupepete au kwa kutumia maji safi peke yake hivyo kubakiwa na mbegu nzito na zilizojaa vizuri.

Jinsi ya kupembua mbegu kwa kutumia maji safi pamoja na chumvi

Mahitaji: - Chumvi kilo 2, Maji lita 10, Yai la kuku, Kijiti cha kukorogea - Chombo cha kupembulia na kuwekea mbegu (ndoo, beseni).



Mbegu zilizoatamishwa kwa masaa 48

Jinsi ya kupembua:

-Changanya maji na chumvi kisha koroga vizuri

-Weka yai kwenye maji ya chumvi

Kama yai litaelea juu ya maji ina maana kuwa mchanganyiko unafaa. Kama halikuelea ongeza kiasi cha chumvi.

-Toa yai na weka mbegu kwenye maji yenye chumvi

-Koroga kwa kijiti na acha maji yatulie na mapepe yaelee juu

-Ondoa mapepe na endelea kukoroga na kuondoa mapepe mpaka yaishe

-Osha mbegu kwa maji safi mara tano ili kuondoa chumvi

-Loweka mbegu kwa kutumia maji safi

Madhumuni ya kuloweka mbegu ni kuiwezesha mbegu kunyonya maji ya kutosha ili iweze kuchipua kabla ya kusia kwenye kitalu.

Jinsi ya kuloweka mbegu:

Kuna njia mbili za kuloweka mbegu (1) Kuloweka mbegu kwenye maji kwa siku nne (4) mfululizo huku ukibadilisha maji, (2) Kuloweka mbegu kwenye maji kwa masaa 24 yaani siku moja na baadaye kutolewa na kuatamishwa kwa masaa 48. Katika njia hizi mbili, njia ya kuloweka mbegu mfululizo kwa siku nne ndiyo inayopendekezwa. Njia hii imeonekana ni bora zaidi kutokana na sababu zifuatazo:-

- Mbegu zote huota kwa pamoja
- Hata kama siku zitazidi kabla



Mbegu ambazo hazikuatamishwa

ya kusia kwenye kitalu hakutakuwa na madhara kwani ukuaji wa mbegu ni wa polepole.

- Hakuna uwezekano wa mche midogo kuvunjika wakati wa kusia kwenye kitalu hasa wakati wa kufunika mbegu kwa kupigapiga na viganja.

- Usiaji wa mbegu kwenye kitalu huwa ni rahisi kwani mbegu huwa hazina mizizi iliyoshikamana.

Mambo ya kuzingatia:

Maji yabadilishwe kila baada ya masaa 12 kwani ni muhimu ili mbegu isioze kwa kukosa hewa. Baada ya masaa 12, hewa safi iliyopo kwenye maji inakuwa imekwisha kwa hiyo ni muhimu kuweka maji mengine ili kufanya mbegu zipate hewa safi ya kutosha na ziendeele kuota. Unashauriwa kuondoa mbegu kwenye maji siku ya nne. Ni muhimu usubiri kwa muda ili maji yote yachuruzike na mbegu ziwe kavu tayari kwa kusia kwenye kitalu.



Wakulima viongozi na wa kati wakijifunza kupembua mbegu za mpunga kwa kutumia maji yaliyotiwa chumvi.